# BAADHI YA VIPINGAMIZI VYA KIUTAWALA VYA KUTUMIA KISWAHILI KUFUNDISHA SEKONDARI NA VYUO

M.M. Mulokozi

**Ikisiri**

Makala hii inaeleza kwa undani jinsi vipingamizi vya kiutawala vinavyokwamisha juhudi za kutumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia shule za sekondari na vyuo. Vipingamizi hivyo ni pamoja na migogoro ya sera, ukosefu wa msukumo wa kisiasa na kisheria, kasumba, udhaifu wa vyombo vya kukuza Kiswahili na shinikizo kutoka nje. Pia, makala inatoa mapendekelezo kadhaa ili Kiswahili kiweze kutumika kama lugha ya kufundishia katika sekondari na vyuo. Baadhi ya mapendekezo hayo ni; utekelezaji wa programu ya mwaka 1999, kuanzisha shule chache za sekondari za majaribio zitakazotumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kuunda sheria zitakazohimiza matumizi ya Kiswahili. Aidha, marekebisho ya katiba yazingatie umuhimu wa Kiswahili kama lugha ya Taifa na matatizo ya asasi mbalimbali zinazohusika na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili yashughulikiwe kitaifa hususani kwa kuongeza bajeti katika asasi hizo.

## 1.0 Utangulizi

Wakati wa ukoloni wa Kiingereza Kiswahili kilitumika kufundishia elimu ya msingi hadi darasa la sita. Kuanzia mwaka 1968, Kiswahili kilifanywa kuwa lugha ya kufundishia elimu yote ya msingi. Kiingereza kingeendelea kutumika kufundishia elimu ya sekondari hadi mwaka 1974; baada ya hapo Kiswahili pekee kingetumika (Tanzania: *Mpango wa Pili wa Miaka Mitano* 1969). Hivyo matarajio ya serikali katika awamu ya kwanza yalikuwa ni kwamba Kiswahili kingechukua nafasi ya Kiingereza kama lugha ya kufundishia sekondari na vyuo kuanzia miaka ya sabini. Kwa bahati mbaya hilo halikuwa. Tume ya Makwetta mwaka 1982 ilipendekeza lugha ya kufundishia iwe Kiswahili, lakini serikali haikutekeleza pendekezo hilo. Rasimu ya Sera ya Lugha ya mwaka 1988 iliyotolewa na Wizara iliyokuwa ikisimamia utamaduni wakati huo ilipendekeza Kiswahili kiwe lugha ya kufundishia, lakini sera hiyo haikupitishwa (Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Utamaduni, Vijana na Michezo 1988). Mwaka 1997 Sera ya Utamaduni iliyoandaliwa na Wizara ya Elimu na Utamaduni ilipitishwa na serikali na Bunge. Miongoni mwa mapendekezo ya sera hiyo ni lile la kutumia Kiswahili kufundishia elimu katika ngazi zote. Kifungu cha 3.4.1 cha sera hiyo kinasema:

> Mpango maalumu wa kuiwezesha elimu na mafunzo katika ngazi zote kutolewa katika lugha ya Kiswahili utaandaliwa na kutekelezwa.
> (Wizara ya Elimu na Utamaduni, *Sera ya Utamaduni*, uk. 19).

Mkutano wa sekta ya utamaduni uliofanyika Arusha tarehe 24-28 Mei, 1999, ulipendekeza ratiba ya utekelezaji wa sera hiyo. Kuhusu lugha ya kufundishia, mkutano ulipendekeza hatua za maandalizi zianze ili Kiswahili kianze kutumika katika kidato cha I kabla ya kupita miaka mitano kuanzia 1999. Wakati haya yakifanyika, Rais wa Awamu ya tatu, Mh.

Benjamin Mkapa, alitoa mwito kwa wananchi kuendelea kujadili suala la lugha ya kufundishia, siyo kutekeleza mageuzi yaliyokwisha amuliwa.
Mapendekezo na maamuzi yote haya hayajatekelezwa kutokana na sababu au vipingamizi mbalimbali. Makala hii itachunguza vipingamizi hivyo, hususani vile vinavyohusiana na utawala, na pale inapowezekana mapendekezo yatatolewa kuhusu hatua zinazofaa kuchukuliwa. Vipingamizi tutakavyovijadili ni vitano:

1. Migongano ya sera
2. Kukosa msukumo wa kisiasa na kisheria
3. Kasumba
4. Udhaifu wa vyombo vya kukuza Kiswahili
5. Shinikizo kutoka nje

Makala itahitimishwa kwa kujaribu kujibu swali la "Tufanye nini" ili tuweze kuvishinda vipingamizi hivi na kutekeleza azma yetu ya kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia elimu ya ngazi zote nchini Tanzania.

## 2. Migongano ya Sera

Tangu enzi za ukoloni hadi leo, Tanzania imefuata sera ya lugha mbili za kufundishia. Lugha moja, Kiswahili, kwa madarasa ya chini, na lugha nyigine, Kiingereza, kwa madarasa ya juu (sekondari na kuendelea). Sera hii imekuwa ni kikwazo cha utekelezaji wa sera ya kutumia Kiswahili tu kwa sababu ya mazoea. Watekelezaji wamezoea lugha ya Kiingereza na baadhi yao walihofu kuwa mabadiliko ya lugha ya kufundishia yangevuruga elimu. Kilichotakiwa ni kutamka tangu mwanzo kwamba sera ya lugha mbili ni ya mpito tu wakati tunajiandaa kutumia Kiswahili pekee.

Tokeo mojawapo la sera hii ya lugha mbili ni kwamba ingawa katika shule nyingi za sekondari walimu na wanafunzi wanatumia Kiswahili ili kuelewana, lakini bado wanalazimika kuandika madondoo ya masomo na mitihani kwa lugha ya Kiingereza. Hivyo wapo wanafunzi wengi wanaoyamudu masomo yao kwa Kiswahili lakini wanashindwa mitihani kwa sababu hawawezi kujibu maswali kwa lugha ya Kiingereza, na hawaruhusiwi kujibu kwa lugha ya Kiswahili.

Mgongano wa sera unajitokeza pia kati ya sera ya utamaduni na sera ya elimu. Ingawa kwa wakati huu sera zote mbili ni za wizara moja ya Elimu na Utamaduni, lakini ukweli ni kwamba zinagongana: sera ya utamaduni inasema tutumie Kiswahili katika ngazi zote za elimu, lakini sera ya elimu inasema tutumie Kiswahili hadi darasa la saba na vyuo vya walimu tu. Zamani masomo kadha ya sekondari yalikuwa yanafundishwa kwa lugha ya Kiswahili kisera; masomo hayo ni Kiswahili chenyewe na Elimu ya Siasa. Siku hizi, baada ya "mageuzi", wizara imerejesha somo la "Uraia" badala ya "Siasa", na kuamua lifundishwe kwa lugha yaKiingereza badala ya Kiswahili.

Mgongano mwingine wa sera vilevile unaihusu Wizara ya Elimu na Utamaduni. Mpaka dakika hii sera rasmi ya lugha ya kufundishia katika shule za msingi nchini Tanzania ni Kiswahili, lakini utekelezaji wa sera hiyo umeanza kuwa wa kibaguzi; baadhi ya shule, hasa za umma, zinalazimika kufuata sera hiyo, na baadhi, hasa za watu binafsi, zimeruhusiwa

kutumia lugha ya Kiingereza kufundishia kuanzia ngazi ya chekechea hadi darasa la saba. Hapa hatuzungumzii shule za kimataifa, ambazo malengo yake kwa vyovyote yatakuwa tofauti na malengo ya shule za Kitanzania; tunazungumzia shule za Kitanzania za kulipia. Baadhi ya shule hizo, au "Akademia" kama zinavyopenda kujiita, zinajitangaza kuwa ni za kimataifa, japo umataifa wao hauonekani, mbali na kutumia lugha ya Kiingereza na kuwaimbisha watoto pembejezi za Kiingereza. Kwa hakika shule hizo zinafundisha watoto wa Kitanzania, siyo wa kigeni, na hivyo zinapaswa kuwaandaa watoto hao walitumikie taifa hili hapo baadaye. Ni hatari kwa watoto wa ngazi hii kuelimishwa katika mfumo ambao hauwajengei msingi imara wa utaifa wao, ambao ni pamoja na lugha, utamaduni na maarifa na maadili ya kitaifa.

## 3.0 Kukosa msukumo wa kisiasa na kisheria

Kipingamizi kingine cha juhudi za kukifanya Kiswahili kiwe lugha ya kufundishia ni ukosefu wa msukumo wa kisiasa na kisheria. Wadachi na Waingereza walipoamua kutumia Kiswahili kufundishia elimu ya ngazi za chini, walikuwa wamefanya uamuzi wa kisera na waliupa msukumo wa kisiasa, ndiyo maana ulifanikiwa. Halikadhalika, Waingereza walitoa msukumo wa kisiasa kwa matumizi ya Kiingereza kufundishia elimu ya sekondari, na msukumo huo ulijitokeza katika sera, mitaala ya ualimu na bajeti pia. Serikali ya awamu ya kwanza ilitoa msukumo wa kisiasa katika matumizi ya Kiswahili kufundishia elimu ya msingi, na katika shughuli za utawala, jeshi na siasa. Hivyo utekelezaji ulifanyika haraka na kwa mafanikio. Leo hili tunapoona majina ya ofisi, vyeo vya kikazi, mitaa, makampuni, n.k yameandikwa kwa lugha ya Kiswahili, na tunapofuatilia mijadala ya wabunge bungeni kwa lugha hiyo, tunasahau kuwa mambo hayakuwa hivyo wakati tulipopata uhuru. Mathalan, mwaka 1961 Mtanganyika wa kawaida asingaliweza kuingia bungeni au kufuata mijadala ya Bunge kwa kuwa lugha iliyotumika ingekuwa ngeni kwake. Hivyo mabadiliko ya lugha yaliyofanywa miaka ya sitini, yakiongozwa na Marehemu Mwalimu J.K. Nyerere na Mh. Rashid Mfaume Kawawa, yalikuwa ni ya kimapinduzi na matunda yake tunayaona leo. Mafanikio ya maamuzi hayo ya kisiasa yaliwezekana tu kutokana na msukumo wa kisiasa ambao serikali na chama tawala cha wakati huo viliutoa.

Kwa bahati mbaya, msukumo huo wa kisiasa haupo tena. Serikali (kwa maana ya viongozi wakuu wa serikali, mbali na uongozi wetu wa "Utamaduni" ambao ndio kazi yao), haisimamii tena kwa karibu na kuzipa msukumo juhudi za kukuza Kiswahili. Aidha, vyama vya siasa havijihusishi kabisa na sera ya lugha katika manifesto zao. Ni viongozi wachache wa vyama wamelizungumzia suala hili, na karibu wote wamekikataa Kiswahili. Mathalan Dkt. Che-Mponda aliwahi kutamka kuwa iwapo chama chake kitashika hatamu, atahakikisha kuwa lugha ya Kiingereza inatumika kufundishia ngazi zote za elimu na katika shule zote. Kadhalika, Dkt. Masumbuko Lamwai aliwahi kutamka bungeni kuwa haifai kutafsiri sheria kwa lugha ya Kiswahili. Kwa upande wa viongozi wa chama tawala, ambao pia ni viongozi wa serikali, Rais Mkapa alitamka hivi karibuni kuwa suala la lugha ya kufundishia lijadiliwe na wananchi. Ingawa kauli hiyo inaonekana kuwa ya kidemokrasia,

lakini haitoi msukumo wa kisiasa, maana inaturudisha kwenye miaka ya 1970-1990, ambapo mijadala mingi ilifanywa magazetini, redioni na katika makongamano kuhusu suala hili. Kwa kweli tunachohitaji wakati huu si mijadala, bali utekelezaji wa uamuzi wa kutumia Kiswahili. Na tunachokihitaji kutoka serikalini ni ratiba ya utekelezaji, bajeti na msukumo wa kisiasa.

Kwa upande wa sheria, mpaka sasa ukuzaji wa Kiswahili haujapewa msukumo wa kisheria. Sheria Kuu ya nchi, yaani Katiba, haitamki kuwa Kiswahili kitakuwa lugha ya taifa na lugha rasmi za shughuli za serikali na elimu. Na hakuna sheria yoyote inayotamka hivyo. Kwa hiyo mtu akiamua kutotumia Kiswahili katika elimu au shughuli yoyote nyingine hawezi kudhibitiwa kisheria. Kwa mfano, tangu watu binafsi waruhusiwe kuanzisha vituo vya redio na televisheni, hakuna sheria ya kitaifa iliyowekwa ili kuwaongoza upande wa matumizi ya lugha na maonyesho ya utamaduni wa Kitanzania kwa jumla. Katika nchi nyingi, ikiwemo Marekani, wenye vituo vya redio na televisheni hubanwa na sheria kutangaza asilimia fulani ya vipindi vyao kwa lugha ya taifa, na pia hulazimishwa kufasiri asilimia fulani ya vipindi vya kigeni katika lugha ya taifa kabla ya kuvionyesha. Kumbe hapa kwetu mambo ni holela tu, kila mtu anajifanyia anavyotaka; anaweza akaamua kutotumia Kiswahili kabisa na asichukuliwe hatua yoyote.

Kukosekana kwa msukumo wa kisiasa na kisheria kumekwamisha maandalizi ya awali ya kukiwezesha Kiswahili kitumike kufundishia sekondari na vyuo. Mathalan, hakuna mipango ya kuandaa walimu wa kutosha wa lugha hiyo, na kuwapiga msasa walimu waliopo ili waweze kuyamudu mabadiliko ya lugha ya kufundishia. Hakuna programu kamili ya kuandika, kufasiri na kuchapisha vitabu vya kiada vya masomo yote ya sekondari na vyuo; na hakuna mipango ya kuandaa wafasiri na wakalimani. Kinachojitokeza ni hali inayofanana na mgomo baridi ndani ya serikali wa kukataa au kuogopa kutekeleza maamuzi yake yenyewe!

## 4.0 Kasumba

Tatizo la "kasumba" lipo, ingawa siku hizi halizungumzwi. Hili ni tatizo la Mwafrika mweusi duniani kote. Chanzo chake ni kutawaliwa kisiasa, kitamaduni, kiuchumi, kidini, kielimu, n.k. Hili ni tatizo kubwa kuliko tunavyodhani, na sidhani kama tunafanya juhudi ya kutosha ya kupambana nalo. Mathalan, katika dunia ya leo ni Mwafrika pekee anayeikataa rangi yake na kujitahidi kuichubua ili kupunguza weusi, ni Mwafrika pekee anayekataa lugha yake, dini yake ya asili, mavazi, tekinolojia, hata majina ya kabila au taifa lake, na kukimbilia kuiga mambo ya wengine. Tatizo hili ni la kiitikadi na kisaikilojia, na haliwezi kutatuliwa bila mapambano makali katika nyanja zote na ngazi zote za utamaduni, elimu, dini, falsafa, lugha, burudani, sanaa, na hatimaye siasa na uchumi.

Mtanzania mwenye kasumba hawezi kukuza Kiswahili, na lazima atapendelea Kiingereza, kwa sababu anaamini kuwa kuongea Kiingereza ndio kuelimika, kuendelea au kustaarabika. Neno "kustaarabika" halina maana ya kuwa kama Mwarabu tu, bali lina maana ya kuwa kama Mzungu pia. Kwa bahati mbaya, mtu mwenye kasumba aghalabu huiga mabaya

badala ya mazuri kutoka kwa "bwana wake", na yake mazuri huyaacha na kubakiza yale mabaya.

Kasumba inatufanya tuwe waoga na tusijiamini. Ndio maana viongozi wetu na wasomi wetu walio wengi wanathubutu kutamka kuwa haiwezekani kutumia lugha ya Kiafrika kufundishia, maana baadhi yao wanaamini kwa dhati kuwa Mwafrika "ni duni" na hivyo lugha yake pia "ni duni". Njia pekee ya kufuta uduni huo ni kujaribu kwa kila hali kuwa kama "Mzungu" au "Mwarabu" au "Muirani".

Tatizo la kasumba upande wa lugha tunaliona katika msimamo wa baadhi ya watu wenye madaraka ya kufanya maamuzi, ambao wanakataa kabisa kukubali Kiswahili kitumike kufundishia kwa madai ya kuwa "hakijakomaa" na "hakitakomaa", au kwa visingizio vya umataifa, kuwania tekinolojia, ukosefu wa fedha, n.k. Tatizo hili tunaliona shuleni ambako leo hii, mwaka wa 2000, watoto bado wanapigwa viboko kwa sababu ya kuongea Kiswahili au lugha zao za kikabila katika eneo la shule. Tunaliona miongoni mwa wanafunzi (na hata wazazi) ambao hawawezi kuongea sentensi moja sahihi ya Kiingereza lakini bado wanataka wafundishwe kwa lugha ya Kiingereza.Yaani wako radhi kuikosa elimu kwa sababu ya kutojua lugha inayotumika kuliko kuipata kwa lugha yao ya taifa ambayo wanaifahamu vizuri!.

Mwenendo wa sasa ulimwenguni ambao tumeuita "utandawazi" *(globalization)* unasaidia kushadidia kasumba ambayo tayari tunayo. Utandawazi kwa Mwafrika si "kutandawana", bali ni "kutandawazwa"; sisi tunakokotwa tu kuingizwa kwenye ulimwengu na utamaduni wa wengine, hususani wa Magharibi, na hatutakiwi kuchangia chochote katika kuumba ulimwengu mpya wa kitekinolojia na kitamaduni. Ndio maana tunashabikia "Manchester United" badala ya timu za nchi kama China au India; tunafurahia burudani kutoka Hollywood na Ulaya, na kufuatilia kwa makini habari na kashfa za wanasiasa na wababe wa huko badala ya habari za kwetu; tunatumia silabasi za Uingereza kufundishia watoto wetu katika "akademia" za bandia badala ya kutumia silabasi za Kitanzania, au angalao za nchi zilizoendelea zaidi kitekinolojia kuliko Uingereza; tunapokea na kushabikia wahubiri wa dini wa madhehebu ya kila aina kutoka Ulaya na Asia, lakini hatujiulizi kwa nini wahubiri Waafrika wa dini zetu za jadi, na hata wa hizi za kigeni tulizoletewa, hawashabikiwi sana huko Ulaya na Asia. Tunafurahia na kujivunia miundo mipya ya magari kutoka Japan, Ulaya na Korea wakati sisi wenyewe hata kiwanda chetu cha baiskeli tumeshindwa kukiendesha na kukiuza kwa wageni.

Kwa ufupi, kila Mwafrika wa leo ana kiasi fulani cha kasumba. Kwa bahati mbaya, wale walio katika ngazi za uongozi mara nyingi ndio wenye kasumba zaidi kwa sababu ya mazingira yaliyowakuza, elimu walioyoipata, mtindo wao wa maisha na nafasi walizo nazo. Kwa kuwa watu hao ndio waamuzi wa masuala ya sera, ikiwemo sera ya lugha na utamaduni, ni wazi kuwa kasumba yao ni kipingamizi kikubwa cha utekelezaji wa sera ya lugha ya kufundishia.

Kasumba ya wakubwa mara nyingi hufungamana na tatizo la ujuaji. Kwa kawaida viongozi wa kisiasa na kiserikali wakitaka kufanya maamuzi kuhusu jambo zito la kisera huwasiliana kwanza na wataalamu wa uwanja unaohusika na kupata ushauri wao. Lakini katika suala la lugha kila kiongozi ni mtaalamu, hawapendi na hawatafuti ushauri wa wataalamu wa kweli

wa uwanja huo, ambao ni wanaisimu na wataalamu wa elimu. Ujuaji wao unachukua nafasi ya ujuzi.
Ni wazi kuwa tunahitaji kuwa na ibara za kisheria kuhusu matumizi ya lugha hapa nchini, kuanzia katika Katiba ya nchi, hadi katika sheria zinazohusu shughuli na vyombo mbalimbali vya umma na vya binafsi, yakiwemo mashirika, shule, vyombo vya habari, shughuli za biashara, n.k. Mathalan, liwe ni kosa la jinai kwa mtu kusambaza nchini Tanzania bidhaa isiyokuwa na maelezo katika lugha ya Kiswahili kwenye ganda lake. Sheria kama hiyo si muhimu katika kutunza heshima ya taifa tu, bali pia ni muhimu kwa usalama na uhai wa walaji.

## 5.0 Udhaifu wa asasi za kukuza Kiswahili

Kikwazo kingine cha utekelezaji wa sera ya kutumia Kiswahili kufundishia ni udhaifu wa vyombo vyenye jukumu la kukuza Kiswahili. Kwa bahati Tanzania ina vyombo vingi vyenye jukumu hilo, vikiwemo:

Radio Tanzania
1952
Wizara inayosimamia Utamaduni
1962
Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili (TUKI)
1964
Shirika la Uchapishaji Vitabu Tanzania (TPH)
1966
Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA)
1967
Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
1968
Shirika la Uchapishaji Vitabu la Afrika Mashariki-EAPL (1948)
1977
Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar (TAKILUKI)
1978
Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA)
1986

Asasi hizi ni mbali na vyama na vikundi vya wananchi wenyewe, kama vile vyama vya Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania (UKUTA), Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania (UWAVITA), Chama cha Wachapishaji wa Vitabu Tanzania (PATA), n.k.
Ili sera ya kutumia Kiswahili itekelezwe vilivyo, lazima vyombo vyote hivi vihusishwe na vifanye kazi yao kwa ufanisi unaotarajiwa. Kwa bahati mbaya uzoefu umeonyesha kuwa vyombo hivi havijafanikiwa kutekeleza wajibu wao kikamilifu, ama kwa sababu ya ukosefu wa fedha na nyenzo, ama kwa sababu nyinginezo. Mathalan, BAKITA, mkuzaji mkuu wa Kiswahili, kwa kipindi kirefu lilikuwa likipewa fedha za kulipia mishahara tu na huduma ndogondogo, na hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake halisi. Matokeo ya hali hii ni kwamba "Baraza" kwa hakika halipo, waliopo ni watendaji tu, maana wajumbe wa Baraza

hawajakutanishwa kwa zaidi ya miaka 15!. Isitoshe, licha ya ukata huo uliokithiri, BAKITA kwa kipindi fulani lilikabiliwa na matatizo ya uongozi na tuhuma za ufujaji wa fedha.

Taasisi ya Elimu nayo halikadhalika haikubadilisha muhtasari wa somo la Kiswahili kwa zaidi ya miaka 20. Hivyo shule zetu zilikuwa zinafundisha Kiswahili cha miaka ya 1960 mwaka 1990!

Mashirika ya umma ya uchapishaji na usambazaji wa vitabu yamekufa au kuuawa kimya kimya. EAPL halipo tena, na haijulikani mali zake lililozirithi kutoka EALB zinatumikaje na kwa manufaa ya nani; TPH linakaribia kukata roho na maiti yake kuuzwa kwa mchawi atakayeihitaji; BAKIZA linaishi kwa kubahatisha, n.k. Kwa jumla, hali ya mashirika ya Kiswahili, isipokuwa machache yanayojimudu, inasikitisha.

Iwapo kweli tunataka Kiswahili kiwe lugha ya kufundishia, itabidi TET waandae silabasi za masomo yote na miongozo ya walimu kwa Kiswahili, TUKI waandae vitabu vya sarufi na makamusi, na tafsiri za vitabu vya taaluma mbalimbali, BAKITA waadae istilahi za kutosha na wasimamie mpango mzima wa utekelezaji, na TPH na DUP na mashirika ya uchapishaji ya binafsi yaandae na kuchapisha vitabu vya masomo yote yanayohusika, n.k. Bali hali halisi inaonyesha kwamba baadhi ya asasi hizi hazitaimudu kazi hiyo. Hivyo hatuna budi kujiuliza: Je, tutaweza kweli kukifanya Kiswahili kiwe lugha ya kufundishia bila kuimarisha asasi za kutekeleza uamuzi huo?

## 6.0 Shinikizo kutoka nje

Uamuzi wa kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia, kama uamuzi mwingine wowote wa kujikomboa, haukosi kuwaudhi wale waliokuwa wakinufaika na hali iliyopo. Kuhusu suala la lugha ya kufundishia, ni wazi kuwa wenye kunufaika tunapoendelea kutumia Kiingereza ni Waingereza na labda Wamarekani. Mwingereza anafahamu fika kuwa Kiingereza ndiyo raslimali yake kuu duniani, na kwa usahihi kabisa anakitetea na kukiendeleza dunia nzima, na asingependelea kuona matumizi yake yanapunguzwa popote pale ulimwenguni.

Kama hivyo ndivyo, hapana shaka kuwa taifa hili kubwa litafanya kila njia kuzishinikiza nchi ndogo zisikitupilie mbali Kiingereza, na kwa kweli ndivyo lifanyavyo kwa njia za wazi na za kificho. Mataifa mengine makubwa, mathalan Ufaransa, halikadhalika yanazishinikiza nchi zenye kutumia lugha zao ziendelee kufanya hivyo. Mathalan, uhusiano kati ya Ufaransa na Rwanda siku hizi umedorora kwa sababu kadha, ikiwemo ile ya watawala wapya wa Rwanda kupendelea kutumia Kiingereza zaidi katika shughuli zao.

Jibu la tatizo hili ni kusimama imara kutetea uhuru wetu na haki yetu ya kujiamulia mambo yetu wenyewe, na kukubali kuyakabili matokeo ya msimamo huo (ambayo yanaweza kuwa machungu).

## 7.0 Hitimisho

Makala hii imejadii baadhi ya vikwazo vya kiutawala vinavyokwamisha utekelezaji wa uamuzi wa kutumia Kiswahili kufundishia elimu ya sekondari na vyuo. Vikwazo vilivyozungumziwa ni: Migongano ya sera; ukosefu wa msukumo wa kisiasa na kisheria; kasumba, na ujuaji unaotokana na kasumba; udhaifu na kutelekezwa kwa vyombo vya kukuza Kiswahili; na mwisho, shinikizo kutoka nje ya nchi. Ili kuweza kuyakabili na kuyashinda matatizo haya, ingefaa hatua zifuatazo zichukuliwe haraka:

7.1 Programu ya utekelezaji wa Sera ya Utamaduni iliyoandaliwa Arusha ianze kutekelezwa kwa dhati kama ilivyopendekezwa, na hili lijitokeze katika bajeti ya serikali ya 2000/2001.

7.2 Tarehe ya kuanza kutumia Kiswahili kufundishia Kidato cha I itangazwe rasmi ili mipango ya utekelezaji ianze.

7.3 Sera ya kutumia Kiswahili kufundishia shule zote za msingi izingatiwe na shule zote (isipokuwa chache ambazo ni za kimataifa hasa). Serikali isimamie utekelezaji wa sera hii na iwachukulie hatua wanaoikiuka.

7.4 Iwapo serikali bado inasita kutumia Kiswahili kufundishia, basi ziteuliwe shule chache za majaribio kila mkoa ambazo zitatumia Kiswahili tu kuanzia kidato cha 1 hadi cha 4; shule hizo zipewe walimu wa kutosha na vifaa vyote vinavyohitajiwa, halafu tathimini ya mafanikio yao ifanywe baada ya miaka 4.

7.5 Marekebisho ya Katiba yazingatie umuhimu wa Kiswahili kama lugha ya Taifa.

7.6 Zitungwe sheria zenye kuhimiza matumizi ya Kiswahili katika vyombo vya habari, sinema na video, mahakama, n.k.

7.7 Asasi za kukuza Kiswahili zitengewe bajeti maalumu kutokana na bajeti ya serikali, fedha za bahati nasibu, n.k. Aidha, asasi zenyewe pia ziwe na mikakati ya kujiongezea mapato.

7.8 Uongozi wa asasi za kukuza Kiswahili uteuliwe kwa uangalifu sana.

7.9 Matatizo ya mashirika ya uchapishaji vitabu yashughulikiwe kitaifa kwa mashauriano na sekta hiyo.

7.10 Mashirika ya taifa ya uchapishaji vitabu, hususani TPH na EAPL, yasiuzwe kwa wageni ambao hawana uchungu na maendeleo ya lugha na fasihi ya Kiswahili.

Mwisho, na muhimu zaidi, msukumo wa kisiasa bado unahitajika. Msukumo huo haupaswi kutoka kwa serikali tu, bali pia kwa vyama vya siasa, na vyama vya hiari vya wakuzaji wa Kiswahili. Ni wajibu wetu sisi wakuzaji wa Kiswahili kuvishinikiza vyama vya siasa na serikali kukienzi na kukiza Kiswahili. Mathalan, tunaweza kuvitaka vyama vya siasa viwe na kipengele kuhusu lugha katika manifesto zao, na kukataa kuvichagua vyama ambavyo havitakuwa na sera nzuri ya kukuza matumizi ya Kiswahili. Halikadhalika, tunaweza kuviomba vyama viishinikize serikali kuharakisha mpango wa kutumia Kiswahili kufundishia sekondari iwapo serikali itaonekana kuzorota. Wakati huo huo, tunawajibika kuendelea kuwaelimisha wananchi kwa jumla kupitia vyombo vya habari, makongamano na vitabu, kuhusu umuhimu wa kutumia lugha ya taifa katika elimu ili waweze kutuunga mkono katika mapambano haya ya kisiasa na kidemokrasia.

## NYARAKA MUHIMU ZILIZOREJELEWA

**Tanzania** 1969 *Second Five Year Development Plan 1969/70 - 1963/74.* Government Printer, Dar es Salaam.

**Tanzania** 1984 *Educational System in Tanzania Towards the Year 2000: Recommendations of the 1982 Presidential Commission on Education as Approved by the Pary and Government (Makweta Report).* Government Printer, Dar es Salaam.

**Tanzania** 1988 "Sera ya Lugha" (rasimu). Idara ya Sanaa na Lugha, Dar es Salaam.

**Tanzania** (hakuna tarehe: 1997?) *Sera ya Utamaduni*. Wizara ya Elimu na Utamaduni, Dar es Salaam.

**Tanzania** 1999 *Ripoti ya Mkutano wa Taifa wa Sera ya Utamaduni.* Wizara ya Elimu ya Utamaduni, Dar es Salaam.